



**Na Mzee
Clark G. Gilbert**
Wa Sabini

RAFIKI KWA RAFIKI

Shangwe ya Kujifunza

Sikuhi kama nilikuwa mwanafunzi mzuri sana wakati ninakua. Ndugu zangu wote walikuwa wazuri sana shulenii. Walipata alama nzuri za ufaulu. Wao walichukua madarasa magumu zaidi. Niliendelea kujaribu madarasa magumu zaidi, lakini sikukubaliwa. Hisabati ilikuwa ngumu sana. Hivyo, niliwaza, "Vyema, nadhani mimi siko vizuri." Sikudhani kama ningeweza kubadilika.

Kisha mwaka mmoja nilipata mwalimu ambaye alinipa kujiamini nillikohitaji. Mwalimu wangu aliona kipaji ndani yangu kuliko mimi nilivyoona. Alisema, "Clark, wewe unaweza kuwa mwanafunzi mzuri. Unahitaji tu kujiamini mwenyewe."

Hivyo, niliendelea kujaribu. Nilijifunza kwa bidii. Pia nilifanya kazi ya kuwa mtu mwenye utaratibu. Nilijifunza kukumbuka kazi zangu za kufanya nyumbani. Kuzima TV kulinisaidia kufokasi kwenye kazi zangu za shule. Punde,

nikawa mwanafunzi bora. Na kujiamini kwangu kukakua.

Nilipokwenda katika misheni yangu, Niliona kwamba sikuhitajika kujifunza peke yangu. Nilimwomba Baba wa Mbinguni kwa ajili ya usaidizi. Na nilimsikiliza Roho Mtakatifu. Kadiri nilivyofanya kazi kwa bidii, niliweza kufundisha na kuwasaidia watu. Niliporudi nyumbani kutoka katika misheni yangu, nilienda chuoni. Niliomba msaada wa Mungu katika kila darasa. Nikawa mwanafunzi bora na hata nikaanza kupenda somo la hisabati.

Nilifikiri kwamba kuwa mzuri shulenii kulimaanisha kwamba wewe unajua mengi sana na shule ilikuwa rahisi kwako. Hiyo siyo kweli. Kama uko tayari kumshirikisha Bwana katika kujifunza na kufanya kazi kwa bidii ili kujiboresha, wewe ni mzuri!

Kama mambo ni magumu sasa hivi, kumbuka kwamba wewe ni mtoto wa Mungu. Unao uwezo wa ajabu. Unaweza kufanya mambo magumu! Endelea tu kufanya mazoezi. Sali kwa Baba wa Mbinguni kwa ajili ya usaidizi. Yeye anataka wewe ufanikiwe. Unaweza kufanya hili! ●

Kutoka kwenye mahojiano ya Olivia Kitterman na Noelle Lambert Barrus.



Kujifunza Burudani

Tafuta kila sampuli ya vifaa vya shule katika miraba iliyoko hapa chini. Unapenda kujifunza kuhusu nini shulenii?



VIELEZO NA AGNES SACCANI

"Tafuteni kutoka kwenye vitabu vizuri maneno ya hekima, tafuteni maarifa hata kwa kujifunza na pia kwa imani;
(Mafundisho na Maagano 109:7).